## KINGO

Na James Gayo






# Kuandaa maisha ya wagonjwa wa akili baada ya matibabu



Wafanyakazi wa TEWWY wakifanya usafi katika kituo cha kurekebisha wagonjwa wa akili kilichopo Temeke Dar es Salaam. Picha na Elias Msuya

INATOKA UK 25

"Zamani nilikuwa nikifanya biashara ya mazao kwa kununua kwa wakulima na kuuza sokoni. Nataka nikitoka hapa nifungue duka la rejareja niejiendeleze na biashara zangu ili kuepuka upweke ambao ndiyo chanzo cha ugonjwa huu."

Mbali na Juma, Alice Mussa (si jina lake halisi) anasema alianza kuugua miaka saba iliyopita alipokuwa akimaliza kidato cha sita katika moja ya shule za sekondari jijini Dar es Salaam.

"Nilifanya mitihani yangu nikiwa wodini. Matokeo yalipotoka nilikuwa na daraja la tatu, ambalo kwangu lilikuwa ni kufeli kwa sababu nilikuwa nikishika nafasi ya kwanza," anasimulia.

Alice anasema bado ndoto yake haijafa.

"Nataka nikitoka hapa niendelee na masomo, nipate shahada ya kwanza, kisha nisome shahada ya pili ili niwe mtetezi wa wagonjwa wa afya ya akili," anasema.

Anasema atawatetea wagonjwa wa afya ya akili kwa sababu wamesahaulika katika jamii na ugonjwa huo haupewi kipaumbele.

"Nataka nibadilishe mtazamo wa jamii kuhusu wagonjwa wa akili. Nataka niwaambie watu kuwa hata mgonjwa wa akili anaweza kupona na kufanya maajabu. Anaweza kuwa mwalimu au daktari au kuwa na familia," anasema.

Anasema wagonjwa wa akili wamekuwa wakinyanyapaliwa tangu ngazi ya familia, jamii na Serikali.

"Hata ukiangalia katika Hospitali ya Muhimbili, magonjwa mengine yanapewa kipaumbele. Magonjwa kama kisukari, moyo utaona wagonjwa wamejengewa majengo mazuri, lakini wodi ya wagonjwa wa akili si sana," anasema.

Ameiomba Serikali kuongeza juhudi za kuwahudumiwa wagonjwa wa akili kwa kutoa ufahamu kwa wananchi na kuongeza wataalamu na miundombinu.

Akikizungumzia kituo cha Vikuruti, muuguzi aliyetambulisha kwa jina la Mwangu Esae anasema kwa sasa kina wagonjwa 11, wanaume wakiwa sita.

"Ili mgonjwa afikishwe hapa, kwanza anapimwa na jopo la madaktari na maofisa ustawi wa jamii ili kuona kama ameimarika kiafya. Kisha mgonjwa mwenyewe na ndugu zake wanaulizwa; wakiridhia ndiyo analetwa hapa," anasema.

Anasema kituo hicho kina uwezo wa kuchukua wagonjwa 32, lakini mara nyingi wagonjwa hufikia kati ya 18 hadi 20.

"Wagonjwa wanachangia Sh3,000 kama ada, Sh18,000 ya malazi na Sh12,000 ya ushauri. Wagonjwa hutakiwa kuishi hapa kwa kati ya miezi mitatu hadi tisa kulingana na kuimarika kwa afya zao. Hata hivyo, wanaweza kuendelea kuishi zaidi kama hawajapona," anasema muuguzi huyo.

Anasema endapo mgonjwa anataka kuondoka kwa hiari yake wanamshauri aage, lakini akitoroka huripotiwa polisi ambako hupewa namba ya kuripoti (RB) ili atafutwe na pia ndugu zake hufahamishwa.

Hata hivyo, alisema kituo hicho hakipokei waathirika wa dawa za kulevya kwa kuwa hakuna miundombinu ya kuwahudumia.

Kwa upande mwingine, daktari wa vitendo, Dawson Muntara anasema wagonjwa wanapofikishwa kituoni hapo hufundishwa kazi ili waweze kujitegemea.

"Kwenye jamii zetu tumeshazoea kuwalemaza wagonjwa kwa kuwafanyia kila kitu. Lakini wagonjwa wakifika hapa tunawafundisha kazi," anasema Muntara.

"Kuna vitendo vya aina tatu wanavyojifunza; kwanza ni kujimudu wenyewe kama vile kuoga, kupiga mswaki, kufua nguo na kuvaa vizuri, pili tunawafundisha kazi za uchumi kama kulima bustani na kufuga na tatu tunawafundisha burudani.

"Kuna burudani ya moja kwa moja kama vile kuimba, kucheza au kupiga ala za muziki na pia kuna zisizo za moja kwa moja kama vile kuangalia luninga au kusikiliza redio," anasema.

Benno Michael, ambaye ni ofisa mifugo wa kituo hicho, anasema hiyo ni miongoni mwa shughuli za kiuchumi wanazofundishwa kwa lengo la kuwawezesha kujitegemea baada ya kuruhusiwa kuondoka kituoni.

"Hapa tunafuga kuku na ngombe. Lengo ni kuwaonyesha wagonjwa jinsi ya kujitegemea kiuchumi kuliko kuitegemea jamii ambayo huishia kuwanyanyapaa na kuwatenga," anasema Michael.

TEWWY iliwatembelea wagonjwa hao kwa lengo la kuwatia moyo katika siku ya kimataifa ya wagonjwa wa akili.

Mkurugenzi mkuu wa TEWWY, Rustica Tembele anasema wamefika kituoni hapo kuwatia moyo wagonjwa kwa kufanya usafi na kuwapa zawadi.

Anasema lengo lao ni kuionyesha jamii kuwa ugonjwa wa akili upo na kuna haja ya kupambana nao kwa kuwapa busara vijana wanaotingwa na msongo wa mawazo.

"Kwetu sisi afya ya akili ni kila kitu. Kama huna afya hiyo, huwezi kuishi. Lengo letu ni kuifanya jamii izungumze kuhusu afya ya akili na jinsi ya kupambana na msongo wa mawazo," anasema.

Anasema walipata wazo la kuanzisha shirika hilo baada ya kuangalia mfumo uliokuwa ukitumika nchini Zimbabwe ambako wazee walikuwa wakizungumza na vijana kuhusu msongo wa mawazo na kuwasaidia kuepukana nao.

"Tuliona kuna haja ya kufanya hivyo nchini, tukaandika wazo na kulipeleka Hivos (Shirika la Misaada la Uholanzi) ambako tumepata ufadhili kufanya kazi hii," anasema.

"Kila siku tunasikia watu wanajiua kwa sababu ya msongo wa mawazo, madeni, wivu wa kimapenzi, umasikini na sababu nyinginezo. Tunataka kuwa suluhisho, tuzungumze na watu hasa vijana tutafute suluhisho la maisha yao," anasema.

**USULI**

**Shirika la Afya Duniani (WHO) linakadiria kuwa watu wenye matatizo ya akili ni takriban asilimia 13 ya maradhi duniani na theluthi moja ya magonjwa yanayohusishwa na ulemavu.**

**Wakati shirika hilo likibainisha kuwepo kwa vitendo vya unyanyapaa na kupuuzwa kwa watu hao, linataja pia changamoto ya huduma duni za afya ikiwa ni pamoja na ukosefu wa wafanyakazi wa afya wenye ujuzi pamoja na ukiukwaji zaidi wa haki zao.**